

TANGAZO KWA UMMA

MWITO WA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA MAREKEBISHO YA BEI ZA MAJI KUTOKA MAMLAKA YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA LINDI (“LUWASA”) KWA MWAKA 2017/18 – 2019/20

Maombi ya mabadiliko ya Bei Na. TR-W-17-012

Mnamo tarehe 11 Septemba 2017, Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ilipokea ombi lililokamilika kutoka Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Lindi (LUWASA) la kutaka kuongeza bei ya huduma zake za majisafi kwa mwaka 2017/18 hadi 2019/20. Jedwali namba 1 hadi 5 hapa chini yanaonesha mchanganuo wa bei za sasa na zinazopendekezwa.

Jedwali 1: Bei za Maji kwa Wateja Walio na dira, za sasa na zinazopendekezwa (Shilingi kwa mita moja ya ujazo).

Aina za Wateja	Bei za sasa	% Ongezeko	Bei zilizopendekezwa		
	2016/17		2017/18	2018/19	2019/20
Majumbani	950	26%	1,200	1,200	1,200
Taasisi	1,100	36%	1,500	1,500	1,500
Biashara	1,400	29%	1,800	1,800	1,800
Viwanda	1,600	25%	2,000	2,000	2,000
Boza	2,300	-	2,300	2,300	2,300
Magati	20	50%	30	30	30

Jedwali 2: Bei za Maji kwa Wateja Wasio na dira, za sasa na zinazopendekezwa (Shilingi Kwa Mwezi).

Aina za Wateja	Bei za sasa	% Ongezeko	Bei zilizopendekezwa		
	2016/17		2017/18	2018/19	2019/20
Majumbani	9,500	5%	10,000	10,000	10,000
Taasisi	19,000	32%	25,000	25,000	25,000
Biashara	32,000	19%	38,000	38,000	38,000
Viwanda	42,000	14%	48,000	48,000	48,000

Jedwali 3: Tozo za Huduma ya Sasa na Iliyopendekezwa (Shilingi kwa Mwezi).

Aina za Wateja	Tozo za sasa	% Ongezeko	Tozo zilizopendekezwa		
	2016/17		2017/18	2018/19	2019/20
Majumbani	2,500	20%	3,000	3,000	3,000
Taasisi	2,500	20%	3,000	3,000	3,000
Biashara	2,500	20%	3,000	3,000	3,000
Viwanda	3,400	18%	4,000	4,000	4,000

Jedwali 4: Ada za Kuunganishiwa Maji za Sasa na Zinazopendekezwa (Shilingi kwa Maunganisho).

Aina za Wateja	Ada za sasa	% Ongezeko	Ada zilizopendekezwa		
	2016/17		2017/18	2018/19	2019/20
Majumbani	30,000	33%	40,000	40,000	40,000
Taasisi	40,000	25%	50,000	50,000	50,000
Biashara	40,000	25%	50,000	50,000	50,000
Viwanda	40,000	50%	60,000	60,000	60,000

Jedwali 5: Ada za Kurejeshewa huduma baada ya kukatiwa za Sasa na Zinazopendekezwa (Shilingi kwa Kurejeshewa huduma).

Aina za Wateja	Ada za sasa	% Ongezeko	Ada zilizopendekezwa		
	2016/17		2017/18	2018/19	2019/20
Majumbani	10,000	50%	15,000	15,000	15,000
Taasisi	40,000	13%	45,000	45,000	45,000
Biashara	40,000	13%	45,000	45,000	45,000
Viwanda	40,000	13%	45,000	45,000	45,000

Kutokana na wasilisho la LUWASA, bei mpya zitaiwezesha kufanikisha mipango ya kuboresha huduma kwa wateja kwa kuongeza uzalishaji wa maji kutoka mitat za ujazo 1,706 kwa siku kwenda mita za ujazo 5,456 kwa siku.

Kwa mujibu wa kifungu Na. 19 (2) (b) cha Sheria Na. 414, kutakuwa na Mkutano wa Taftishi siku ya **Alhamisi, tarehe 23 Novemba, 2017 katika Ukumbi wa Double M katika Manispaa ya Lindi** kuanzia saa **10:00 asubuhi** kwa ajili ya kupata maoni ya wadau ikiwa ni pamoja na Baraza la Ushauri la Serikali na Baraza la Ushauri la Watumia Huduma zinazodhibitiwa na EWURA na wananchi wote kwa ujumla kuhusu uhalali wa bei zinazopendekezwa.

Wadau wanaopenda kutoa maoni kwa maandishi wanaombwa kufanya hivyo kwa kutuma maoni yao kwa Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kwa anuani iliyoonesha hapo juu kabla ya tarehe **28 Novemba, 2017**. Maelezo zaidi yanaweza kupatikana katika ofisi ya EWURA, **GHOROFA YA SABA, LAPF PENSIONS FUND TOWER; MKABALA NA KIJIKI CHA MAKUMBUSHO, KIJITONYAMA, DAR ES SALAAM** au ofisi za LUWASA, MKOA WA LINDI.

Imetolewa na:

**Kaimu Mkurugenzi Mkuu
Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA)
03 Novemba 2017**